

AMKA HAUJACHELEWA

Kanuni ya kukupa
matokeo ndani ya siku 21

Daniel Mwita

AMKA HAUJACHELEWA, FANIKISHA....FANIKIWA!

Je umekwama kimaisha? Umekwama kifedha? Unahisi kupoteza matumaini?

Jibu lako ni **NDIO?**

Uko sehemu sahihi na uamuzi wa kusoma kilichoandikwa humu ni hatua ya kwanza katika kutatua changamoto zako.

Hatua za kitabu hiki kifupi nazo pia ni fupi na zinazotekelezeka.

Ukianza kuzifuata maisha yako yataanza kubadilika siku baada ya siku, mwezi baada ya mwezi na mwishowe mafanikio, furaha na amani vitakuwa vyako.

Karibu sana, anza safari hii njema.

MAHUSIANO NA WATU NA VITU

Upo katika hali uliyopo kwa sababu ya mahusiano yako na watu na vitu bila kujali idadi yake.

Mfano umepoteza kazi kwa sababu ya mahusiano mabaya na **kitu** kama pombe ukawa mlevi ikaleta athari katika utendaji wa kazi, hatimaye mahusiano mabaya na **mtu au watu** katika kazi.

Mahusiano mabaya na **muda** yanapelekea kuwa nje ya ratiba na mipango kisha unapoteza **nafasi** nyingi za kukunufaisha.

Kama ni kilimo umechelewa mvua, kuvuna na soko. Kama ni shule unapata ufaulu hafifu au kufeli,

Kama ni mapenzi ndoa inavunjika, au unaoa mke au kuolewa na mwanaume ambae hajawa tayari (msumbufu)

Mifano mingine unaweza kutafakari mwenyewe.

✓ **Zoezi la kwanza;**

Tafakari mahusiano mabaya yaliyokufikisha ulipo, kisha tafakari mahusiano mabaya uliyo nayo sasa, anza na orodha ya watu kisha orodha ya vitu.

YA KALE YAMEPITA

Unaposoma kuanzia hapa elewa kuwa yaliyopita yamepita ni muda wa kuachana nayo na kuepuka athari za moja kwa moja kutokana na mambo yaliyopita.

Acha kuogopa na kujipa wasiwasi juu ya mambo ambayo bado hayajatokea hasa mambo hasi.

Acha kuwaza na kujihukumu kwa mambo ambayo yamepita;

Kauli kama “sitapatakazi, mke, mume, pesa, rafiki, mpenzi, nyumba kama ile ACHANA NAZO

ACHANA na watu wabinafsi wasiotaka na wewe ufanikiwe, katika mambo yako. Hata kama wana mafanikio.

RUHUSU hali ya kukubali KUACHANA na mambo hayo yanayokuathiri, maumivu yake ni ya muda kisha **UTAVUNA** mafanikio, amani na furaha baada ya wakati fulani

✓ **Zoezi la pili;**

Acha kusononeka kuhusu ndoa iliyoshindikana, mke aliekukimbia, pesa ulizopoteza, marafiki waliokudharau au unaodhani

wanakudharau. Kuanzia unaposoma mpaka hapa katika nukta mwisho wa sentensi hii **HAYO NI MAMBO YALIYOPITA.**

HAJI BETRI YAKO

Ulipokuwa mtoto miaka tuseme kati ya 7 hadi 12 na zaidi kidogo, katika utendaji wa mambo yako unayoyapenda au uliyoamua kufanya unakumbuka ilikuwaje?